## Carta de Cristina Koga

Estudia 2º de Secundaria, tengo 15 años. Nací en el pueblo de Maduma en la provincia de Iringa. En mi familia somos cuatro hermanos. Mis padres murieron. Vivimos con mi abuela y una tía, trabajan el campo y somos muy pobres.

Quiero agradecer a Dios la oportunidad de poder estudiar en el colegio de Educa y también quiero agradecer a las personas de Educa que nos dan todo lo que necesitamos además de la educación para conseguir un futuro mejor.

Me gusta mucho este colegio de Educa por el ambiente, se puede estar estudiar tranquilamente, tiene aulas con mesas y sillas, luz eléctrica, y otras muchas cosas como el uniforme, los libros, cuadernos, jabón, la comida. También el colegio es bonito y cómodo el sitio para dormir y si estoy enferma me llevan al hospital.

Me gustaría estudiar hasta llegar a la Universidad porque quiero ser médico, y así ayudar a mi familia.

Doy las Gracias a todos los de Educa y os pido que no os canséis.

24-10-2018:

HISTORIA YA MAISHA YANGU

Kwa jina ninaitwa Christina Koga, natokea ~~Shule ya Sekondari~~ Kata ya Maduma iliyopo wilaya ya Mufindi mkoa wa Iringa. Nina umri wa miaka kumi na tano.

Katika familia yetu tupo watoto wanne(4) lakini wazazi wote wawili hawapo walisha tangulia mbele za haki. Mimi ni mtoto wa tatu katika familia nina kaka mmoja ambaye ni mkulima, nina dada mmoja ambaye bado anasoma kidato cha nne pia nina mdogo wangu mmoja ambaye yupo darasa la nne. Tangu wazazi wangu walipo toweka duniani tumekuwa tukiishi na bibi yetu ambaye walisaidiana na mama yetu mkubwa katika kutulea na kutupa mahitaji mbalimbali na hao wote hawana kazi maalumu ila zaidi ni wakulima tu, kwa kweli maisha ya nyumbani ni magumu kidogo.

Napenda kumshukuru Mungu kuniwezesha kupata nafasi hii ya kusoma shule ya Educa na pia napenda sana kuwashukuru Mama Pilarr na wenzake kwa kuanzisha shule hii ili sisi tupate huduma hii ya elimu. Shule hii ya Educa nimeipenda kwa sababu ina mazingira mazuri katika kujisomea, yaani madarasa ambayo yana viti, meza pamoja na mwanga na pia ni shule ambayo ipo sehemu tulivu na pia nimeipenda kwa sababu mahitaji yote tunayapata hapa hapa shuleni kama vile sare za shule, daftari, peni, sabuni, miswaki na dawa, sehemu nzuri ya kulala na mtu akiumwa anapelekwa hospitalini.

Sababu ya kutokuwa shule niliyotoka na kufika Educa, kwanza ni umbali kutoka shule niliyokuwa ninasoma hii ilikuwa ni sababu moja wapo ya kuto fika shuleni siku zingine na kubakia nyumbani na pia sababu ya kuja shule ya Educa na siyo shule zingine, ni kwamba shule zingine zina gharama ambazo walezi wangu wapo chini ya uwezo, na ikawa mtu anayeitwa Braitoni ali ye tutafutia hii shule na hapa shuleni nililetwa na kaka yangu anaye itwa Izack. Naendelea kushukuru kwa kuipata shule hii nzuri ambayo tunapatia haki yetu ya elimu. Mungu aendelee kuwazidishia nguvu msikate tamaa ya kuendelea kutusaidia.

Nina penda kusoma hadi kufika chuo kikuu kisha Mungu akinijalia niwe Daktari. Ni matumaini yangu kwamba nitakamilisha ndoto zangu. Katika shule hii nitahakikisha nasoma kwa bidii na ninafaulu katika mitihani yangu yote kwa lengo la kukamilisha ndoto zangu.